لَآاِلٰـهَ اِلَّا اللّٰهُ مُحَمَّدٌ رَّسُوْلُ اللّٰهِ

اِنَّ الدِّيْنَ عِنْدَ اللّٰهِ الْاِسْلَامِ

# MAOMBI YA MTUME MTUKUFU MUHAMMAD (S.A.W.)

# اَدْعِيَةُ الرَّسُوْلِ

صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمُ

**Kimeenezwa na Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya (TANZANIA)**

**S.L.B. 376, Dar es Salaam**

**Simu +255 22 2111031**

© Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania

Chapa ya Kwanza 1971

Chapa ya Kumi na Tano 2023

Kimepigwa chapa na Ahmadiyya Printing Press

S.L.P. 376, Dar es Salaam

وَاِذَا سَاَلَكَ عِبَادِىْ عَنِّىْ فَاِنِّىْ قَرِيْبٌ ط

اُجِيْبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ اِذَا دَعَانِ فَلْيَسْتَجِيْبُوْالِىْ

وَلْيُؤْمِنُوْا بِىْ لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُوْنَ ط

"Na watu Wangu watakapokuuliza juu Yangu,
basi hakika Mimi Nipo karibu.
Nayaitikia maombi ya mwombaji anaponiomba,
basi waniitikie na waniamini, ili wapate
kuongoka".
(Kurani Tukufu 2: 187)

*Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.*

## NENO LA MBELE

Miezi michache iliyopita niliweza kukusanya MAOMBI YA KURANI TUKUFU na kuyapigisha chapa pamoja na tafsiri yake kwa Kiswahili. Kitabu hicho, kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu, kilipokelewa vizuri na nakala elfu tatu za Maombi zilitoka katika muda mdogo na zikaenea Uganda, Kenya na Tanzania.

Kwa kuwa Kiswahili hakisemwi sana na wananchi wa Uganda, ndugu wa hapa walipenda tafsiri ya Kiganda pia itoke ya maombi hayo yenye baraka. Kazi hiyo pia ilifanyika na sasa ndugu hao wanaona raha kwa kusoma tafsiri ya maombi hayo kwa kikwao. Mwenyezi Mungu Awapokelee maombi yao na kuwaongezea nuru mioyoni mwao.

Baadaye, jamaa wengine na Wabashiri wa Kenya na Tanzania waliniomba niwatolee kitabu

kingine juu ya Maombi ya Mtume Mtukufu Muhammad (SAW). Na sasa, Alhamdulillahi, naona furaha kukiweka mbele yenu. Kitabu hiki, kwa hakika, kilipata kupigwa chapa zamani; lakini maombi ya Kiarabu namna yalivyotamkwa na Mtukufu Mtume (SAW) hayakuwamo. Ingawaje tafsiri ya maombi vile vile ilisaidia watu wengi, lakini wale waliokuwa na ujuzi wa Kiarabu hawakuona utamu hasa kwa sababu ya kukosekana maneno ya Kiarabu.

Nilipoanza kutafuta maneno hayo ndani ya vitabu vya Hadithi nilikuta kazi ngumu; maana maombi yalikuwa yametolewa katika vitabu mbalimbali. Ilitaka jitihada kubwa kuzitafuta hizi Hadithi mpaka nikafanikiwa kupata maombi yote na kuyapanga sawa na madhumuni yake. Pamoja na kutafuta mengi ya yale maombi ya zamani nimeongeza mengine niliyoyakuta ndani ya vitabu na sasa kitabu hiki kimekuwa kama kitabu kipya cha maombi.

Ugumu mwingine ulikuwa wa kutafsiri maombi hayo kwa Kiswahili. Nikiwa huku Uganda Kiswahili chanipiga chenga na kujaribu kuniponyoka Katika kutunga kitabu hiki nimesaidiwa na kile cha kwanza chenye tafsiri tupu kilichotungwa na Maulana Sheikh Mubaraka Ahmad H.A. Hususan namshukuru ndugu yangu mpenzi Maulana Sheikh Muhammad Munawwar H.A., Mbashiri wetu Mkuu nchini Tanzania, ambaye alisoma na kusahihisha muswada wote wa kitabu hiki.

Mwenyezi Mungu Ampokelee juhudi yake na pia Anibariki juhudi yangu na kitabu hiki akifanye chenye manufaa makubwa kwa Waislamu wote na kuwaangaza kwa mwanga usiyo na kifani wa Mtume Mtukufu Muhammad (SAW). Amin.

Mtumish wa Uislamu,
Sheikh Muhammad Ishaque Soofi,
Msikiti wa Ahmadiyya,
Jinja, Uganda.
12 Rabiul Awwal 1391 H. Qamariyyah.

## HAKIKA YA SALA NI MAOMBI

Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu ya Ahmadiyva, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad, amani ya Mungu iwe juu yake, ameandika haya katika makala yake iliyosomwa kama hotuba mjini Sialkot, Pakistan, juu ya maombi: "Msidhani ya kuwa sisi vile vile tunaomba kila siku na sala tunayosali ni dua tu. Kwa sababu yale maombi ambayo hupatikana baada ya kupata maarifa na fadhila huwa na rangi na kaifiya ya namna nyingine. Hayo ni kitu chenye kuangamiza, ni moto unaolainisha na kunyenyekeza, kina mvuto kama ule wa sumaku ambacho kinajivutia rehema. Hicho ni kifo lakini mwishowe huleta uzima; ni tufani kali ingawa baadaye inageuka kuwa safina. Kila jambo lililoharibika hupata kutengenezwa kwa maombi na kila aina ya sumu inabadilika kuwa dawa iponyeshayo kwa ajili yake.

"Wamebarikiwa wale wafungwa ambao huomba, wala hawachoki; kwa maana siku moja watatoka gerezani. Wamebarikiwa wale vipofu ambao hawalegei katika kuomba; maana siku moja watapata kuona. Wamebarikiwa wale walalao ndani ya makaburi ambao wanatafuta msaada wa Mungu kwa maombi; maana siku moja watatolewa ndani ya makaburi.

"Mmebarikiwa ninyi ikiwa hamchoki kwa kuomba, na roho zenu huyeyuka kwa sababu ya maombi na macho yenu hutiririsha machozi na huwasha moto vifuani mwenu na kukuchukueni hadi vyumba vyenye giza na mapori yasiyokaliwa na watu ili mpate ladha ya kuomba faraghani; na hukufanyeni mkose utulivu na kuonekana kama wenda wazimu msiojitambua; kwani hatimaye mtaona fadhili za Mwenyezi Mungu. Yule Mungu Ambaye mimi ninakuitieni mumtafute ni Mkarimu, Mwenye kurehemu, Mwenye kuona

haya, Mkweli, Mwaminifu na Mwenye kuhurumia wanyonge. Na ninyi, kadhalika, muwe waaminifu sana na mkamwombe kwa ukweli hasa na usafi kamili wa nia; ndipo Atakurehemuni. Jitengeni na kelele za dunia, wala msitie kwenye dini rangi ya magomvi yenu ya ubinafsi. Kubalini kushindwa kwa kumridhisha Mwenyezi Mungu na pokeeni ushinde kwa furaha ili mrithi ushindi ulio mkuu. Waombao, Mwenyezi Mungu Atawaonyesha mwujiza; na wenye kutaka watapewa neema isiyo ya kawaida.

Maombi hutoka kwa Mwenyezi Mungu na hurudia kwake. Kwa sababu ya  maombi Mungu Anakuwa karibu sana na mwanadamu kama roho yako ilivyo karibu sana na mwili wako.

Baraka ya kwanza ya maombi ni kwamba mtu anapata badiliko takatifu ndani mwake. Kisha kwa sababu ya badiliko hilo Mungu vilevile

Anabadili sifa Zake: Ingawa sifa za Mwenyezi Mungu hazibadiliki, lakini yule aliyebadilika anaona onyesho la pekee la sifa Zake ambazo watu wa dunia hii hawalijui. Yaonekana kana kwamba ni Mungu mwingine asiyekuwa huyu wa zamani, kumbe siye mwingine ila ni Yuleyule tu; isipokuwa onyesho jipya Humwonesha katika sura mpya. Hapo, katika hali ile ya onyesho maalumu Mungu Anaonesha kazi za ajabu kwa yule aliyebadilika ambazo Hakuzionesha kwa watu wengine. Hii ndiyo ile miujiza!

"Kwa ufupi maombi ni ile dawa ya ajabu ambayo inabadili gao la mchanga kuwa dhahabu halisi; ndiyo maji ambayo husafisha uchafu wote wa ndani. Kwa sababu ya moambi hayo roho huyeyuka na kutiririka kama maji kumwelekea Mola Aliye wa pekee na kujimwagia huko huko.
Wakati huo roho husimama wima mbele ya Mwenyezi Mungu na kuinama na pia humsujudia.

Na kivuli chake ni ile sala ambayo imefundishwa na Uislamu. Na kusimama kwa roho ni kujiweka tayari kuvumilia kila shida na msiba kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na kutii amri Zake. Na kuinama kwake ni kujitenga na mapenzi na mafungamano ya namna zote na kumwelekea Mwenyezi Mungu na kujifanya kuwa wake tu. Na kusujudu kwake ni kujitupa mbele ya Mwenyezi Mungu na kujipoteza kabisa na kujiangamiza nafsi yake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Hii ndiyo sala ambayo inamkutanisha mtu na Mola wake. Na sheria ya Kiislamu imechukua picha ya sala hiyo ya roho na kuamrisha sala ya kimwili; ili sala ya kimwili ielekeze kwenye sala ile ya roho. Kwa sababu Mwenyezi Mungu Amemtengeneza mwanadamu awe na hali hii ya kuwa roho inaathiri mwili na mwili huathiri roho. Roho yako inapohuzunika, macho hayana budi kutiririsha machozi. Na roho inapofurahi, uso pia huchangamka na kuonyesha dalili ya furaha,

hata pengine mtu huanza kucheka. Kadhalika, mwili ukiumwa au kuumia, roho pia inashiriki shida hiyo. Na mwili unapoona raha kwa sababu ya hewa nzuri, roho vilevile hupata sehemu ya starehe hiyo. Hivyo ibada za kimwili shabaha yake ni kuchochea roho imwelekee Mwenyezi Mungu kwa sababu ya kufungamana na mwili na ili roho pia ishughulike katika kusimama wima na kusujudu." (Uk. 26-28).

## KANUNI ZA KUMUOMBA MWENYEZI MUNGU

1. Sisi Waislamu hatumuombi yeyote ila Mwenyezi Mungu. Kama tutakavyoona katika maombi yote yaliyofundishwa na Mtume wetu Muhammad (SAW) kila ombi lazima lielekezwe kwa Mwenyezi Mungu. Yeye Husikia maombi yetu yote bila maombi hayo kumpitia mtu mwingine. Mwenye kuwaomba wengine katika sala zake, hata wakiwa Manabii, au Mawalii, si Mwislamu.

2. Wakati wa kuomba lazima tuwe na yakini ya kuwa Mwenyezi Mungu Anao uwezo wa kila aina na Anaweza kutusaidia katika mahitaji yetu yote ila yale ambao ni kinyume na sheria Yake. Kwa mfano, tukitaka maiti afufuke arudi duniani akae nasi, hayo ni kupinga sheria ya Mwenyezi Mungu. Jambo hili litatendeka Akhera tu, siyo sasa hivi. Ombi hilo halitapokelewa kamwe.

3. Ombi lolote lililo kinyume na sifa njema za Mwenyezi Mungu, pia halikubaliwi. Tukimuomba Mwenyezi Mungu Aonane nasi ana kwa ana, tumwone kwa macho yetu ya kimwili; hili haliwezekani. Mwenyezi Mungu hana mwili tunaoweza kuuona dhahiri.

4. Tusichoke katika kumwomba Mwenyezi Mungu. Yaani, tukiisha muomba siku kumi au mwezi mmoja na tusione alama ya kupokelewa ombi letu; basi tusikate tamaa na kuacha maombi. Sharti mwombaji aendelee mpaka afanikiwe, au akatazwe na Mwenyezi Mungu asiombe dua hiyo, kwani analoomba lina shari kwake.

5. Kazi ya mja ni kuomba. Tusing'ang'anie kwamba jambo lifanyike kwa sura ileile tulivyotaka. Mwenyezi Mungu ni BWANA na sisi ni watumishi Wake. Tofauti hii tusikubali

isahaulike wakati wowote. Au, itakuwa siyo kuomba; bali kulazimisha. Na hakuna mtu aliyetaka kumlazimisha Mwenyezi Mungu jambo akafanikiwa.

6. Wakati wa kuomba maneno yasisemwe kwa mdomo tu, bali mwombaji aonyeshe unyonge wake na unyenyekevu wake mbele ya Mwenyezi Mungu na kujiona dhaifu sana kwa kulia machozi na kuonyesha mahangaiko ya moyo wake hasa.

7. Mwombaji awe mwenye kutimiza amri za Mwenyezi Mungu na kutii sheria Zake. Maisha ya mtu yakiwa safi bila kuwa na uasi, maombi yake hupokelewa upesi.

8. Mwenye kumuomba Mwenyezi Mungu awe mwenye kufanya jitihada kwa kutimiza jambo hilo analoomba lipatikane. Yule aliye na uwezo wa kufanya juhudi, kisha hafanyi yeye humjaribu Mola wake, wala hataona ufaulu wakati wowote.

Naam, akikatazwa na Mwenyezi Mungu asifanye lolote, bali asubiri tu matokeo ya uwezo na kazi za Mwenyezi Mungu; hapo ni sawa kutofanya jitihada.

9. Wakati wa kuanza maombi, kwanza mwombaji amsifu Mwenyezi Mungu kwa sifa njema na tukufu (kwa kusoma surah ALHAMDU au nyinginezo) kisha amsalie Mtume Muhammad (SAW) (kwa kukariri Sala ya Mtume na maombi mengine); ndipo alete mahitaji yake.

10. Katika kuomba, Mwislamu anaweza kumwomba Mwenyezi Mungu kwa lugha yake mwenyewe; kwani Mwenyezi Mungu Husikia lugha zote. Ni afadhali kutumia kwanza maombi yaliyomo ndani ya Kurani Tukufu au yaliyofundishwa na Mtume Muhammad (SAW) kisha ndio alete maombi kwa lugha yake mwenyewe. Ikiwa haelewi kabisa Kiarabu, hapo itabidi atumie lugha yake mwenyewe na kukaza

kabisa maombi na kurudia rudia na kukaririkariri mpaka mwenyewe anatosheka na moyo unatoa ushahidi kwamba maombi yamefika mahali pake.

11 . Mwombaji aombe sana msamaha wa dhambi zake; maana dhambi hizo pengine zinakuwa pazia kubwa lenye kuzuia maombi yake yasisikilizwe. Hata kama anaomba jambo gani, maghofira lazima yaombwe kwanza ili njia ifunguke, pazia liondoke na maombi yafike katika baraza tukufu la Mwenyezi Mungu.

12. Yafaa sana muombaji atoe mali kuwapa masikini na wenye haja. Ikiwa hana mali, basi amtumikie mwenzake kwa kumtimizia haja yake. Hii pia ni njia ya kuchochea rehema ya Mwenyezi Mungu. Ukimsaidia mwanadamu. mwenzako au kiumbe kingine chenye uhai, msaada wa Mwenyezi Mungu hufanya haraka kuteremka na kukuondolea shida yako.

13. Mtu anaweza kuomba nje ya sala vile vile; lakini nafasi iliyo bora sana ni kuomba mahitaji yako katika sala. Yaani, baada ya kusoma maneno maalumu yanayotakiwa kusomwa ndani ya sala, unaweza kuongeza hayo unayoyahitaji maalumu yawekwe mbele ya Mwenyezi Mungu. Pia unaweza kuongeza hayo kunuia rakaa mbili za nafali ili kuomba unachotaka. Wakati wa baada ya usiku wa manane ndiyo hufaa hasa ambapo unaamka baada ya kulala kidogo kisha unazungumza na Mola wako faraghani bila kuonekana na watu wengine. Ukiwa peke yako unaweza kunyanyua sauti yako kwa kuomba. Hiyo inalainisha sana moyo wako na mshale hupata lengo lake.

14. Unaweza kumwomba Mwenyezi Mungu wakati wowote, lakini ni afadhali utawadhe kwanza ili mwili uburudike nawe uweze kukazia fikira zako vizuri katika dua. Usafi wa mwili kwa

hali yoyote humpendeza Mwenyezi Mungu.

15. Yafaa kuelekea kibla wakati wa maombi ikiwa inawezekana. Kama haiwezekani, basi unaweza kumwomba Mwenyezi Mungu hata kama unatembea au unakimbia au unalima au unafanya, kazi nyingine. Jambo kubwa ni kuelekeza moyo wako upande wa Mola wako. Mambo mengine na masharti mengine ni kukusaidia hali hiyo ya moyo ipatikane.

16. Pengine ombi linakubaliwa kwa njia nyingine usiyoitaka. Hii pia ni rehema ya Mwenyezi Mungu. Uliloomba pengine halikuwa na heri kubwa, au lilikuwa na ubaya fulani ndani yake; basi Mwenyezi Mungu Akakupatia lile lililo jema zaidi kuliko uliloomba.

17. Pengine ombi letu halikubaliwi kwa sura yoyote ili kutujaribu katika imani yetu na

kutegemea kwetu. Hapo inatakiwa subira sana bila kuonyesha hasira au kutokuwa na shukurani. Hata haifai kuwaendea waganga na wapigaji bao. Hilo ni kumvunjia heshima Mwenyezi Mungu na kumfanya mpuuzi machoni petu. Mtume (SAW) amesema maombi yasiyokubaliwa yanawekwa akiba kwa ajili ya mtu huyo naye hupata malipo yake huko Akhera; kwani maombi ni ibada pia. Basi, tusipoteze malipo yetu ya baadaye ambayo tutayahitaji sana siku ya Kiyama.

18. Maombi yetu yasiwe zaidi kwa ajili ya vitu vya dunia tu. Kinachostahili kuombwa sana ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu na ukaribu naye. Masikini wee, itakusaidia nini kupata riziki na mali na watoto na heshima ikiwa hukumridhisha Mola wako? Kapatane na Muumba wako kwanza kisha mambo mengine yataonekana hafifu machoni mwako. Ukiyakosa au ukiyapata, yatakuwa mamoja kwako.

19. Inasaidia pia wakati wa kuomba kutaja sifa ile maalumu ya Mwenyezi Mungu inayohusiana na mahitaji yako. Kwa mfano, unaweza kusema: Ee Razzaq, Uniruzuku; Ee Khaaliq, Unipe mtoto; Ee Ghafuur, Unighofiri; Ee Saattaar, Unisitiri na kadhalika. Ndani ya Kurani Tukufu zimetajwa sifa nyingi za Mwenyezi Mungu kama sura 59, Aya 23-25.

20. Yafaa kupanua ombi lako. Yaani, usijiombee nafsi yako tu, bali uwaombee wengine pia ili rehema ya Mwenyezi Mungu ifurike na kufunika watu wote pamoja na wewe. Kama unapanda ndege, uwaombee salama abiria wote. Na kama unapanda mbegu ndani ya shamba lako uwaombee neema na jirani zako pia.

**(1)**

***Dua kabla ya Kuanza kazi yoyote njema***

١= بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ط

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa Ukarimu.

٢= بِسْمِ اللّٰهِ فِىْ اَوَّلِهٖ وَاٰخِرِهٖ

Ukisahau kuomba dua hiyo ukakumbuka katikati ya kazi, basi, utumie dua hii:

2. Kwa jina la Mwenyezi Mungu, mwanzoni mwa kazi na mwishoni mwake.

**(2)**

***Dua wakati wa kuamka usingizini***

١= اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ الَّذِىْ اَحْيَانَا بَعْدَ مَا اَمَاتَنَا وَاِلَيْهِ النُّشُوْرُ۔

٢= اَللّٰهُمَّ اِنِّیۡ اَسۡئَلُكَ خَیۡرَ هٰذَ الۡیَوۡمِ وَفَتۡحَهٗ وَنَصۡرَهٗ وَنُوۡرَهٗ وَبَرَكَتَهٗ وَهُدٰهُ وَاَعُوۡذُبِكَ مِنۡ شَرِّ مَا فِیۡهِ وَشَرِّ مَا بَعۡدَهٗ ۔

٣ = اَللّٰهُمَّ بِكَ اَصۡبَحۡنَا وَبِكَ اَمۡسَیۡنَا وَبِكَ نَحۡیَا وَبِكَ نَمُوۡتُ وَاِلَیۡهِ النُّشُوۡر ۔

٤ = اَللّٰهُمَّ اجۡعَلۡ اَوَّلَ هٰذَ النَّهَارِ صَلَاحًا وَاَوۡسَطَهٗ فَلَاحًا وَاٰخِرَهٗ نَجَاحًا اَسۡئَلُكَ خَیۡرَ الدُّنۡیَا وَالۡاٰخِرَةِ یَا اَرۡحَمَ الرَّاحِمِیۡنَ ۔

Tafsiri:

1 . Sifa zote njema zinamhusu Mwenyezi Mungu Aliyetuhuisha baada ya kutufisha na Kwake ni ufufuo.

2. Ee! Mola wetu, mimi ninakuomba heri ya siku hii; na ushindi wake na nusura yake; na nuru yake na mwongozo wake; na ninajikinga Kwako na shari iliyomo ndani yake; na itakayokuja

baadaye.

3. Ee! Mola wetu, kwa amri Yako tumepambazukiwa na kufikiwa na jioni; na kwa amri Yako tumepata uzima na kwa amri Yako tutakufa; na Kwake Mwenyezi Mungu watu wote watakusanywa.

4. Ee! Mola wetu, Ufanye mwanzo wa siku hii uwe wa kutengenea na kati yake iwe ufaulu na mwisho wake uwe wokovu. Nakuomba kheri ya dunia na Akhera; ee! Mwenye kurehemu zaidi kuliko warehemuo wote.

**(3)**

***Dua Wakati wa Kwenda Kulala***

١ = بِا سْمِكَ رَبِّىْ وَضَعْتُ جَنْبِىْ فَاغْفِرْلِىْ ذَنْبِىْ۔

٢ = اَللّٰهُمَّ بِا سْمِكَ اَمُوْتُ وَاَحْيٰى۔

٣ = اَللّٰهُمَّ اَسْلَمْتُ وَجْهِيْ اِلَيْكَ وَاَلْجَأْتُ ظَهْرِيْ

اِلَيُكَ وَفَوَّضُتُ اَمُرِيُ اِلَيُكَ رَغُبَةً وَ رَهُبَةً اِلَيُكَ
لَا مَلُجَأَ وَلَا مَنُجٰى مِنُكَ اِلَّا اِلَيُكَ اٰمَنُتُ بِكِتَابِكَ
الَّذِىُ اَنُزَلُتَ وَنَبِيِّكَ الَّذِىٓ اَرُسَلُتَ ـ
٤ = اَللّٰهُمَّ قِنِىُ عَذَابَكَ يَوُمَ تَبُعَثُ عِبَادَكَ

Tafsiri:

1. Ee Mola wangu, kwa jina Lako ninaweka ubavu wangu, basi nighofirie dhambi zangu.

2. Ee Mola wangu, kwa jina Lako ninakufa na kuwa hai.

3. Ee Mola wangu, najisalimisha uso wangu Kwako, na mgongo wangu nauweka katika ulinzi Wako, na jambo langu nakukabidhi Wewe, nikiwa na matumaini Kwako pamoja na kukuogopa. Hakuna kimbilio wala penye wokovu ila Kwako tu. Naamini kitabu Chako Ulichokiteremsha na Nabii Wako Uliyemtuma.

4. Ee Mola wangu niokoe na adhabu Yako siku Utakayofufua watumishi Wako.

**(4)**

***Dua wakati wa kugutuka baada ya kuona ndoto yenye kutisha.***

اَعُوْذُ بِكَلِمَاتِ اللّٰهِ التَّامَّاتِ مِنْ غَضَبِهٖ وَعِقَابِهٖ
وَشَرِّ عِبَادِهٖ وَمِنْ هَمَزَاتِ الشَّيَاطِيْنِ اَنْ يَّحْضُرُوْنَ

Tafsiri:

Najilililida kwa maneno makamilifu ya Mwenyezi Mungu katika ghadhabu, Yake na adhabu Yake na shari ya watu Wake na katika mashawishi mabaya ya mashetani, au wao kunisogelea.

**(5)**

***Dua ya Kupata Mapenzi ya Mwenyezi Mungu***

١ = اَللّٰهُمَّ اِنِّىْٓ اَسْأَلُكَ حُبَّكَ وَحُبَّ مَنْ يُّحِبُّكَ

وَحُبَّ مَا يُقَرِّبُنِیُ اِلَيُكَ۔

٢ = اَللّٰهُمَّ اجُعَلُ حُبَّكَ اَحَبَّ اِلَیَّ مِنُ نَّفُسِیُ وَمَالِیُ وَاَهُلِیُ وَمِنَ الُمَآءِ الُبَارِدِ

Tafsiri:

1. Ee Mola wangu, hakika mimi nakuomba mapenzi Yako na mapenzi ya hao wanaokupenda na mapenzi ya yale yatakayonipeleka karibu Nawe.

2. Ee Mola wangu, Ufanye mapenzi Yako yanivutie zaidi kuliko nafsi yangu na mali yangu na ahali zangu na kuliko maji ya baridi.

**(6)**

***Dua ya kuomba usafi wa moyo na viungo* vingine.**

١ = اَللّٰهُمَّ طَهِّرُ قَلُبِیُ مِنَ النِّفَاقِ وَاَعُمَالِیُ مِنَ الرِّيَاءِ وَلِسَانِیُ مِنَ الُكَذِبِ وَاَعُيُنِیُ مِنَ الُخِيَانَةِ فَاِنَّكَ تَعُلَمُ

خَائِنَةَ الْاَعْيُنِ وَمَا تُخْفِى الصُّدُوْرُ ۔
٢= اَللّٰهُمَّ اِنِّيْٓ اَعُوْذُ بِكَ مِنْ عِلْمٍ لَّايَنْفَعُ وَمِنْ قَلْبٍ لَّا يَخْشَعُ وَمِنْ نَّفْسٍ لَّا تَشْبَعُ وَمِنْ دَعْوَةٍ لَّا يُسْتَجَابُ لَهَا ۔
٣ = اَللّٰهُمَّ زِدْنَا وَلَا تَنْقُصْنَا وَاَكْرِمْنَا وَلَا تُهِنَّا وَاَعْطِنَا وَلَا تَحْرِمْنَا وَاٰثِرْنَا وَلَا تُؤْثِرْ عَلَيْنَا وَاَرْضِنَا وَارْضَ عَنَّا ۔
٤ = اَللّٰهُمَّ اجْعَلْنِىْ شَكُوْرًا وَ اجْعَلْنِىْ صَبُوْرًا وَاجْعَلْنِىْ فِىْ عَيْنِىْ صَغِيْرًا وَفِىْ اَعْيُنِ النَّاسِ كَبِيْرًا ۔

Tafsiri:

1. Ee Mola wangu, Utakase moyo wangu usiwe na unafiki, na matendo yangu yasiwe na riya (kujionyesha), na ulimi wangu usitamke uwongo, na macho yangu yasifanye hiyana. Hakika Wewe Unajua hiyana ya macho na yale ambayo

vifua vinayaficha.

2. Ee! Mola wetu; ninajilinda Kwako na elimu ambayo haifai na kwa moyo ambao hauogopi, na kwa nafsi ambayo haishibi; na kwa maombi ambayo hayakubaliwi.

3. Ee! Mola wetu, Utuzidishe wala Usitupunguze, na Utupe heshima wala Usitufedheheshe; na Utupe wala Usitunyime; na Utupende wala Usiwapendelee (wengine) zaidi kuliko sisi, na Uturidhishe na Uturidhie.

4. Ee! Mola wangu, Unifanye niwe mwenye kushukuru; na mwenye kusubiri; na Unifanye nijione mdogo na machoni mwa watu nionekane mkubwa.

**(7)**

***Dua ya Kujiongezea Elimu***

اَللّٰهُمَّ انْفَعْنِىْ بِمَا عَلَّمْتَنِىْ وَعَلِّمْنِىْ مَا يَنْفَعُنِىْ وَزِدْنِىْ عِلْمًا وَالْحَمْدُ لِلّٰهِ عَلٰى كُلِّ حَالٍ وَاَعُوْذُ بِاللّٰهِ مِنْ عَذَابِ النَّارِ۔

Tafsiri:

Ee Mola wangu, Uninufaishe kwa yale Uliyonifunza, na Unifundishe yenye kuninufaisha, na Uniongezee eiimu. Na sifa zote zinamhusu Mwenyezi Mungu kwa kila hali. Najikinga kwa Mwenyezi Mungu na adhabu ya moto.

**(8)**

**Dua wakati wa kuanza kula**

بِسْمِ اللّٰهِ وَعَلٰى بَرَكَةِ اللّٰهِ

Tafsiri:

Kwa jina la Mwenyezi Mungu na kwa baraka za Mwenyezi Mungu.

**(9)**

***Dua baada ya Kula***

١ = اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ الَّذِىْ اَطْعَمَنَا وَسَقَانَا وَجَعَلَنَا مِنَ

الْمُسْلِمِيْنَ ۔

٢ = اَللّٰهُمَّ بَارِكْ لِیْ فِیْهِ وَاَطْعِمْنِیْ وَاَسْقِنِیْ خَیْرًا مِّنْهُ

Tafsiri:

1. Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu Aliyetulisha na kutunywesha na Akatujaalia tukawa Waislamu.

2. Ee Mola wangu, Unitilie baraka (chakula) hiki na Unilishe na kuninywesha vilivyo bora, kuliko hiki.

## (10)

***Dua ya kumwombea mwenyeji wako.***

اَللّٰهُمَّ بَارِكْ لَهُمْ فِیْمَا رَزَقْتَهُمْ وَاغْفِرْلَهُمْ وَارْحَمْهُمْ

Tafsiri:

Ee Mola wangu, Uwatilie baraka vyote Ulivyowapa na uwaghofirie na kuwarehemu.

## (11)

**Dua wakati unapojitizama katika kioo.**

اَللّٰهُمَّ كَمَا حَسَّنْتَ خَلْقِيْ فَاَحْسِنْ خُلُقِيْ وَحَرِّمْ وَجْهِيَ عَلَى النَّارِ۔

Tafsiri:

Ee Mola wangu, kama Ulivyonipa umbo jema, pia nipe tabia njema na uso wangu Uuharimishie moto.

## (12)

***Dua ya kupata ulinzi wa Mwenyezi Mungu Mahali popote na wakati wowote.***

١ = بِسْمِ اللّٰهِ الَّذِيْ لَا يَضُرُّ مَعَ اسْمِهٖ شَيْءٌ فِى الْاَرْضِ وَلَا فِى السَّمَآءِ وَهُوَ السَّمِيْعُ الْعَلِيْمُ۔

٢ = اَعُوْذُ بِكَلِمَاتِ اللّٰهِ التَّآمَّاتِ مِنْ شَرِّ مَا خَلَقَ۔

٣ = اَللّٰهُمَّ لَكَ الْحَمْدُ اَنْتَ نُوْرُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ

وَمَنْ فِيُهِنَّ وَلَكَ الْحَمْدُ اَنْتَ قَيِّمُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ وَمَـنْ فِيُهِـنَّ وَلَكَ الْحَمْدُ اَنْتَ الْحَقُّ وَوَعْدُكَ الْحَقُّ وَالسَّاعَةُ حَقٌّ وَالنَّبِيُّوْنَ حَقٌّ وَمُحَمَّدٌ حَقٌّ ۔

٤ = اَلـلّٰهُـمَّ لَكَ اَسْـلَـمْـتُ وَعَـلَيْكَ تَـوَكَّلْتُ وَبِكَ اٰمَــنْــتُ وَاِلَيْكَ اَنَبْــتُ وَبِكَ خَــاصَـمْـتُ وَاِلَيْكَ حَـاكَـمْـتُ فَـاغْـفِـرْلِـىْ مَـا قَدَّمْتُ وَمَآ اَخَّرْتُ وَمَآ اَسْـرَرْتُ وَمَـآ اَعْلَنْتُ اَنْتَ الْمُقَدِّمُ وَاَنْتَ الْمُؤَخِّرُ لَآ اِلٰهَ اِلَّآ اَنْتَ وَ لَآ اِلٰـهَ غَيْرُكَ ۔

٥ = اَللّٰهُمَّ اِنِّىْٓ اَسْأَلُكَ مِنْ خَيْرِ مَا سَأَلَكَ مِنْهُ نَبِيُّكَ مُـحَـمَّـدٌ صَـلَّـى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَاَعُوْذُبِكَ مِنْ شَرِّ مَـااسْتَـعَـاذَ مِـنْـهُ نَبِيُّكَ مُحَمَّدٌ صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ وَاَنْـتَ الْـمُسْتَعَانُ وَعَلَيْكَ الْبَلَاغُ وَلَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ اِلَّا بِاللّٰهِ ۔

Tafsiri:

1. Kwa jina la Mwenyezi Mungu Ambaye kwa jina lake hakidhuru chochote katika ardhi wala katika mbingu, naye ni mwenye kusikia sana (maombi ya waja Wake), Mjuzi sana (wa hali yao na mahitaji yao).

2. Najikinga kwa maneno makamilifu ya Mwenyezi Mungu na shari ya Alivyoviumba.

3. Ee! Mola wangu, sifa zote ni Zako Wewe ni nuru ya mbingu na ardhi, na yaliyomo ndani yake. Sifa zote ni zako, Wewe ni Mlinzi wa mbingu na ardhi na yaliyomo ndani yake. Sifa zote Unazo Wewe. U Mkweli; na ahadi Yako ni ya haki; na Saa ile ni haki; na Manabii ni wenye haki; na Muhammad (SAW) ni mwenve haki.

4. Ee! Mola wetu, nimejitupa Kwako na Kwako ninategemea na wewe nakuamini na Kwako nimegeukia. Najadiliana kwa ajili Yako na Kwako naomba hukumu. Basi, Unighofirie niliyoyatanguliza na niliyoyaahirisha; na

niliyoyaficha na niliyoyadhihirisha. Wewe ni Mwenye kutanguliza na Mwenye kuahirisha; hakuna apasaye kuabudiwa ila Wewe na hakuna Mwabudiwa minghairi Yako.

5. Ee! Mola wetu, nakuomba heri yoyote ambayo aliiomba Kwako Mtume Wako Muhammad (SAW); na ninajilinda Kwako na shari yoyote ambayo alikuomba umwepushe nayo Mtume Wako Muhammad (SAW) na Wewe Ndiye Aombwaye msaada na ni juu Yako kuufikisha (Ujumbe) na hakuna nguvu ya kujiepusha na dhambi wala hakuna nguvu ya kufanya mema ila Kwake tu Mwenyezi Mungu.

## (13)

***Dua wakati wa kuvaa nguo mpya.***

١ = اَللّٰهُمَّ لَكَ الْحَمْدُ كَمَا كَسَوْتَنِيْهِ اَسْئَلُكَ خَيْرَهٗ وَخَيْرَ مَا صُنِعَ لَهٗ وَاَعُوْذُبِكَ مِنْ شَرِّهٖ وَشَرِّ مَا صُنِعَ لَهٗ ـ

٢ = اَلْـحَـمْدُ لِلّٰهِ الَّذِيْ رَزَقَنِيْ مِنَ اللِّبَاسِ مَا اَتَجَمَّلُ بِـهٖ فِـى الـنَّاسِ وَاُوَارِىْ بِهٖ عَوْرَتِىْ وَ اَتَجَمَّلُ بِهٖ فِىْ حَيَاتِىْ -

Tafsiri:

Ee Mola wangu, nakusifu, kwa kunivisha (nguo) hii, nakuomba heri yake na heri ya shabaha ya kutengenezwa kwake. Ninakukimbilia Unilinde na shari yake na shari ya shabaha ya kufumwa kwake.

2. Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu Aliyenipatia mavazi ambayo kwayo ninaonekana mzuri kati ya watu, na ambayo kwayo najisitiri aibu yangu na kujipamba katika maisha yangu.

**(14)**

***Dua kubwa kabisa ya kuomba msamaha wa Madhambi***

اَلـلّٰهُـمَّ اَنْـتَ رَبِّىْ لَآ اِلٰـهَ اِلَّآ اَنْتَ خَلَقْتَنِىْ وَاَنَا عَبْدُكَ

وَاَنَـا عَلٰى عَهْدِكَ وَوَعْدِكَ مَااسْتَطَعْتُ اَعُوْذُ بِكَ مِنْ
شَـرِّ مَـا صَنَعْتُ اَبُوْءُ لَكَ بِنِعْمَتِكَ عَلَيَّ وَاَبُوْءُ بِذَنْبِيْ
فَاغْفِرْلِيْ فَاِنَّهٗ لَا يَغْفِرُ الذُّنُوْبَ اِلَّا اَنْتَ ـ

Tafsiri

Ee Mala wangu, Wewe ni mlezi wangu, hakuna anayestahili kuabudiwa ila Wewe. Wewe Uliniumba na mimi ni mtumishi Wako. Ninashika ahadi Yako sawa na uwezo wangu. Nakukimbilia Unilinde na shari ya yale niliyoyatenda. Ninarejea Kwako kwa sababu ya neema Zako na ninakiri makosa yangu; basi Unisamehe dhambi zangu, maana hakuna mwenye kusamehe madhambi ila Wewe tu.

**(15)**

***Dua wakati wa kuingia chooni***

اَللّٰهُمَّ اِنِّيْٓ اَعُوْذُبِكَ مِنَ الْخُبُثِ وَالْخَبَآئِثِ ـ

Tafsiri:

Ee! Mola wangu, nakimbilia Kwako nijilinde na kila uchafu na yanayochukiza.

## (16)

### *Dua wakati wa kutoka chooni*

١ = غُفْرَانَكَ ـ

٢ = اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ الَّذِىْ اَذْهَبَ عَنِّى الاَذٰى وَعَافَانِىْ

Tafsiri:

1. (Naomba) ghofira Yako (Ee Mola wangu).
2. Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu Aliyeniondolea udhia na kunipa afya.

## (17)

### *Dua baada ya kusikia adhana*

اَللّٰهُمَّ رَبَّ هٰذِهِ الدَّعْوَةِ التَّامَّةِ وَالصَّلٰوةِ الْقَائِمَةِ

اٰتِ مُـحَـمَّـدَ اِلْـوَسِيُـلَةَ وَالْـفَضِيُلَةَ وَالدَّرَجَةَ الرَّفِيُعَةَ وَابُـعَثُـهُ مَقَامًا مَّحُمُوُدَا اِلَّذِيُ وَعَدُتَّهٗ اِنَّكَ لَا تُخُلِفُ الْمِيُعَاد۔

Tafsiri:

Ee Mola wangu, Mlezi wa wito huu uliokamilika na sala inayosimama! Mpe Muhammad (SAW) ukaribu na fadhila na cheo kilichonyanyuka na Umfikishe mahali paliposifika ambapo Ulimwahidi; hakika Wewe Huvunji miadi.

**(18)**

***Dua baada ya kuoga au kutawadha***

اَللّٰهُمَّ اجُعَلُنِىُ مِنَ التَّوَّابِيُنَ وَاجُعَلُنِىُ مِنَ الْمُتَطَهِّرِيُنَ

Tafsiri:

Ee Mola wangu, nijaalie niwe miongoni mwa wanaotubu na miongoni mwa wanaojitakasa.

**(19)**

***Dua ya wakati wa kuelekea Msikitini kwa ajili ya sala ya alfajiri.***

اَللّٰهُمَّ اجْعَلْ فِىْ قَلْبِىْ نُوْرًا وَاجْعَلْ فِىْ لِسَانِىْ نُوْرًا وَاجْعَلْ فِىْ سَمْعِىْ نُوْرًا وَاجْعَلْ فِىْ بَصَرِىْ نُوْرًا وَاجْعَلْ مِنْ خَلْفِىْ نُوْرًا وَاجْعَلْ مِنْ اَمَامِىْ نُوْرًا وَاجْعَلْ مِنْ فَوْقِىْ نُوْرًا وَاجْعَلْ مِنْ تَحْتِىْ نُوْرًا اَللّٰهُمَّ اَعْطِنِىْ نُوْرًا

Tafsiri:

Ee Mola wangu, nijaalie nuru moyoni mwangu na katika ulimi wangu na katika masikio yangu na katika macho yangu, na Unijaalie niwe na nuru nyuma yangu na mbele yangu, na juu yangu na chini yangu. Ee Mola wangu, nipe nuru (tupu).

## (20)

***Dua wakati wa kuingia Msikitini.***

بِسْــمِ الــلّٰــهِ الصَّلٰوةُ وَالسَّلَامُ عَلٰى رَسُوْلِ اللّٰهِ اَاللّٰهُمَّ اغْفِرْلِىْ ذُنُوْبِىْ وَفْتَحْ لِىْ اَبْوَابَ رَحْمَتِكَ

Tafsiri:

(Naingia) kwa jina la Mwenyezi Mungu. Rehema na amani ziwe juu ya Mtume wa Mwenyezi Mungu. Ee Mola wangu, nisamehe dhambi zangu na Unifungulie milango ya rehema Zako.

## (21)

***Dua wakati wa kutoka msikitini.***

بِسْــمِ الــلّٰــهِ الــصَّلٰوةُ وَالسَّلَامُ عَلٰى رَسُوْلِ اللّٰهِ اَللّٰهُمَّ اغْفِرْلِىْ ذُنُوْبِىْ وَفْتَحْ لِىْ اَبْوَابَ فَضْلِكَ ـ

Tafsiri:

(Natoka) kwa jina la Mwenyezi Mungu. Rehema na amani ziwe juu ya Mtume wa Mwenyezi

Mungu. Ee Mola wangu, nisamehe dhambi zangu na Unifungulie milango ya fadhili Zako.

## (22)

***Dua katika sala baada ya Thanaa***

١ = اَللّٰهُمَّ بَاعِدْ بَيْنِيْ وَبَيْنَ خَطَايَایَ كَمَا بَاعَدْتَّ بَيْنَ المَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ۔

٢ = اَللّٰهُمَّ نَقِّنِيْ مِنَ الْخَطَایَ كَمَا يُنَقِّى الثَّوْبُ الْاَبْيَضُ مِنَ الدَّنَسِ

٣ = اَللّٰهُمَّ غْسِلْ خَطَايَایَ بِالْمَاءِ وَالثَّلْجِ وَالْبَرَدِ۔

Tafsiri:

1. Ee! Mola wetu, Uniweke mbali na dhambi kama ilivyo mbali Mashariki kutoka Magharibi.
2. Ee! Mola wetu, Unisafishe na hatia kama nguo nyeupe inavyotakaswa na uchafu.
3. Ee! Mola wetu, Ukoshe makosa yangu kwa maji na kwa theluji na kwa barafu.

## (23)

***Dua baada ya Attahiyyatu na sala ya Mtume, kabla ya kutoa salamu.***

١ = اَللّٰهُمَّ اِنِّىْ ظَلَمْتُ نَفْسِىْ ظُلْمًا كَثِيْرًا وَلَا يَغْفِرُ الذُّنُوْبَ اِلَّآ اَنْتَ فَاغْفِرْلِىْ مَغْفِرَةً مِّنْ عِنْدِكَ وَارْحَمْنِىْ اِنَّكَ اَنْتَ الْغَفُوْرُ الرَّحِيْمُ

٢ = اَللّٰهُمَّ اِنِّىْ اَسْأَلُكَ مُوْجِبَاتِ رَحْمَتِكَ وَعَزَآئِمَ مَغْفِرَتِكَ وَالْغَنِيْمَةَ مِنْ كُلِّ بِرٍّ وَالسَّلَامَةَ مِنْ كُلِّ اِثْمٍ رَبِّ لَا تَدَعْ لِىْ ذَنْبًا اِلَّا غَفَرْتَهٗ وَلَا هَمًّا اِلَّا فَرَّجْتَهٗ وَلَا حَاجَةً هِيَ لَكَ رِضًا اِلَّا قَضَيْتَهَا يَا اَرْحَمَ الرَّاحِمِيْنَ ـ

٣ = اَللّٰهُمَّ اَكْفِنِىْ بِحَلَالِكَ عَنْ حَرَامِكَ وَاَغْنِنِىْ بِفَضْلِكَ عَمَّنْ سِوَاكَ ـ

٤ = اَللّٰهُمَّ اِنِّىْٓ اَعُوْذُبِكَ مِنَ الْهَمِّ وَالْحُزْنِ وَ

اَعُوْذُبِكَ مِنَ الْعَجْزِ وَالْكَسْلِ وَ اَعُوْذُبِكَ مِنَ الْجُبْنِ وَالْبُخْلِ وَاَعُوْذُبِكَ مِنْ غَلَبَةِ الدَّيْنِ وَقَهْرِ الرِّجَالِ ـ

٥ = اَللّٰهُمَّ اِنِّىْٓ اَعُوْذُبِكَ مِنَ الْمَأْثَمِ وَالْمَغْرَمِ ـ

٦ = اَللّٰهُمَّ اِنِّىْٓ اَعُوْذُبِكَ مِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ وَاَعُوْذُبِكَ مِنْ عَذَابِ جَهَنَّمَ وَاَعُوْذُبِكَ مِنْ فِتْنَةِ الْمَسِيْحِ الدَّجَّالِ وَاَعُوْذُبِكَ مِنْ فِتْنَةِ الْمَحْيَا وَالْمَمَاتِ ـ

٧ = اَللّٰهُمَّ اِنِّىْٓ اَعُوْذُبِكَ مِنْ جَهْدِ الْبَلَآءِ وَدَرْكِ الشَّقَآءِ وَسُوْٓءِ الْقَضَآءِ وَشَمَاتَةِ الْاَعْدَآءِ ـ

Tafsiri:

1. Ee Mola wangu, nimejidhulumu sana nafsi yangu na hakuna awezaye kusamehe madhambi ila Wewe, basi Unipe maghofira kutoka Kwako

na Unirehemu. Hakika Wewe Ndiwe Msamehevu, Mrehemevu.

2. Ee Mola wangu, nakuomba yale yenye kunivutia rehema Zako na maghofira Yako yaliyo thabiti. Nifunze kutenda kila jema wala nisitende dhambi ya aina yoyote. Ee Mola wangu, Usiache dhambi yangu yoyote bila kuisamehe, wala huzuni yo yote bila kuniondoleayo, wala haja yoyote (ambayo Umeridhia) bila kuitimiza, Ewe Mwenye kurehemu zaidi kuliko warehemuo (wote).

3. Ee Mola wangu, Unitoshelezee kwa riziki Yako iliyo halali, nisiingie vile Ulivyoviharamisha, na Unitajirishe kwa fadhila zako nisimwendee mwingine minghairi Yako.

4. Ee Mola wangu, nakimbilia kwako Unilinde na wasiwasi na huzuni; (tena) nakimbilia Kwako Unilinde na kupungukiwa na uvivu); (tena) nakimbilia Kwako Unilinde na woga na ubahili; na (tena) nakimbilia Kwako Unilinde na

kushindwa na deni na kughilibiwa na watu.

5. Ee Mola wangu, nakukimbilia Unilinde na makosa na kuwiwa.

6. Ee Mola wangu, nakukimbilia Unilinde na adhabu ya kaburi, (tena) nakukimbilia Unilinde na adhabu ya Jahannamu, nakukimbilia (tena) Unilinde na fitina ya mdanganyifu mkuu (Dajjali), (tena) nakukimbilia Unilinde na fitina ya uhai na kifo.

7. Ee Mola wangu nakukimbilia Unilinde na shida kali na bahati mbaya na hukumu isiyoridhisha na maadui kupata furaha.

## (24)

***Dua baada ya Sala***

١ = اَسْتَغْفِرُ اللّٰهَ رَبِّىْ مِنْ كُلِّ ذَنْبٍ وَّاَتُوْبُ اِلَيْهِ ـ

٢ = اَللّٰهُمَّ اَنْتَ السَّلَامُ وَمِنْكَ السَّلَامُ وَاِلَيْكَ يَرْجِعُ السَّلَامُ تَبَارَكْتَ يَا ذَاالْجَلَالِ وَالْاِكْرَامِ ـ

٣ = اَللّٰهُمَّ اَعِنِّیْ عَلٰی ذِكْرِكَ وَشُكْرِكَ وَحُسْنِ عِبَادَتِكَ ۔

٤ = اَشْهَدُ اَنْ لَّآ اِلٰـهَ اِلَّا اللّٰهُ وَحْدَهٗ لَا شَرِيْكَ لَهٗ لَهُ الْـمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ وَهُوَ عَلٰی كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ ۔ اَللّٰهُمَّ لَا مَانِعَ لِمَا اَعْطَيْتَ وَلَا مُعْطِيَ لِمَا مَنَعْتَ وَلَا يَنْفَعُ ذَاالْجَدِّ مِنْكَ الْجَدُّ ۔

٥ = رَبِّ اِنِّیْ ظَلَمْتُ نَفْسِیْ وَعْتَرَفْتُ بِذَنْبِیْ فَاغْفِرْلِیْ ذُنُوْبِیْ فَاِنَّهٗ لَا يَغْفِرُ الذُّنُوْبَ اِلَّآ اَنْتَ ۔

٦ = سُبْحٰنَ اللّٰهِ وَبِحَمْدِهٖ سُبْحٰنَ اللّٰهِ الْعَظِيْمِ

Tafsiri:

1. Ninamuomba msamaha Mwenyezi Mungu, Mola wangu, kwa dhambi zangu zote na ninatubia Kwake.

2. Ee Mola wangu, Wewe ni Mwenye amani na amani hutoka Kwako na hurejea Kwako

U Mwenye baraka, ewe Mtukufu, Mwenye heshima.

3. Ee Mola wangu, Unisaidie nikukumbuke na nikushukuru na nikuabudu vizuri.

4. Nashuhudia kwamba, hakuna mwabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu, pekee Asiye na mshirika; ufalme ni Wake na sifa (pia); Naye Ndiye Mwenye uwezo juu, ya kila kitu. Ee Mola wangu, hakuna mwenye kuzuia Ulichotoa wala hakuna mwenye kutoa Ulichokizuia wala ukubwa wa yeyote haumfai mbeleYako.

5. Ee Mola wangu, nimejidhulumu nafsi yangu na nimekiri makosa yangu; basi Unighofirie madhambi yangu. Hakika, mwenye kusamehe dhambi hakuna ila Wewe tu.

6. Yu Mtakatifu Mwenyezi Mungu pamoja na sifa zake; Yu Mtakaitifu Mwenyezi Mungu, Mwenye adhama.

**(25)**

***Dua wakati wa kuona mwezi***

اَللّٰهُمَّ اَهِلَّهٗ عَلَيْنَا بِالْاَمْنِ وَالْاِيْمَانِ وَالسَّلَامَةِ وَالْاِسْلَامِ رَبِّىْ وَرَبُّكَ اللّٰهُ ـ

Tafsiri

Ee Mola wetu, Utuletee (mwezi mpya) Huu kwa amani na imani na usalama na Uislamu. (Ee mwezi) Mungu wangu Na Mungu wako ni Allah (Mwenyezi Mungu).

**(26)**

***Dua ya Kufunga Saumu***

وَبِصَوْمِ غَدٍ نَوَيْتُ مِنْ شَهْرِ رَمَضَانَ ـ

Tafsiri

Nanuia kufunga saumu kesho katika wezi wa Ramadhani.

**(27)**

***Dua wakati wa Kufuturu***

اَلـلّٰهُـمَّ لَكَ صُـمُـتُ وَبِكَ اٰمَـنُـتُ وَعَلَيُكَ تَوَكَّلُتُ وَعَلٰى رِزُقِكَ اَفُطَرُتُ۔

Tafsiri:

Ee Mola wangu, nilifunga kwa ajili Yako, na Wewe nakuamini, na juu Yako nategemea, na kwa riziki Yako ninafuturu.

**(28)**

***Dua katika usiku wa heshima (Lailatul - Qadri mnamo kumi la mwisho wa Ramadhani.***

اَللّٰهُمَّ اِنَّكَ عَفُوٌّ تُحِبُّ الُعَفُوَ فَاعُفُ عَنِّىُ۔

Tafsiri:

Ee Mola wangu, Wewe ni Msamehevu Unapenda kusamehe; basi nisamehe (dhambi zangu).

**(29)**

***Dua wakati wa kutoa Zaka***

رَبَّنَا تَقَبَّلْ مِنَّا اِنَّكَ اَنْتَ السَّمِيْعُ الْعَلِيْمُ۔

Tafsiri:

Ee Mola wetu, Utupokelee; hakika Wewe ni Mwenye kusikia sana, Mjuzi.

**(30)**

***Dua wakati wa kupiga chafya***

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ

Yaani: Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu.

Anayesikia maneno haya atasema:

يَرْحَمُكُمُ اللّٰهُ

Yaani: Mwenyezi Mungu Akurehemu.

Ndipo mwenye kupiga chafya atajibu:

يَهْدِ يْكُمُ اللّٰهُ وَيُصْلِحُ بَالَكُمْ۔

Yaani: Mwenyezi Mungu Akuongozeni na kutengeneza mambo yenu (yawe mema).

**(31)**

***Dua wakati wa kutoka katika mkutano wa watu***

سُبْحَانَكَ اللّٰهُمَّ وَبِحَمْدِكَ اَشْهَدُ اَنْ لَّآ اِلٰـهَ اِلَّا اَنْتَ اَسْتَغْفِرُكَ وَاَتُوْبُ اِلَيْكَ۔

Tafsiri:

U Mtakatifu, ee Mola wangu, pamoja na sifa Zako. Ninashuhudia kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Wewe. Nakuomba msamaha na ninatubia Kwako.

**(32)**

***Dua wakati wa kwenda sokoni***

بِسْمِ اللّٰهِ اَللّٰهُمَّ اِنِّيْٓ اَسْأَلُكَ خَيْرُ هٰذَ السُّوْقِ وَخَيْرَ مَا فِيْهَا وَاَعُوْذُبِكَ مِنْ شَرِّهَا وَشَرِّ مَا فِيْهَا۔ اَللّٰهُمَّ اِنِّيْٓ اَعُوْذُبِكَ اَنْ اُصِيْبَ فِيْهَا صَفْقَةً خَاسِرَةً۔

Tafsiri

(Ninaingia sokoni) kwa jina la Mwenyezi Mungu. Ee Mola wangu, nakuomba heri va soko hili na heri; ya yote yale yaliyomo ndani, yake. Na ninakuomba Unilinde na shari yake na shari ya yote yale yaliyomo ndani yake. Ee Mola wangu, nakukimbilia Unilinde nisipate hasara katika ununuzi wangu humo.

**(33)**

***Dua kwa kupata ufaulu kazini***

رَبَّنَآ اٰتِنَا مِنۡ لَّدُنۡكَ رَحۡمَةً وَهَيِّئۡ لَنَا مِنۡ اَمۡرِنَا رَشَدًا۔

رَبِّ اشۡرَحۡ لِىۡ صَدۡرِىۡ وَيَسِّرۡلِىۡ اَمۡرِى۔

Tafsiri:

Ee Mola wetu, Utupe rehema kutoka Kwako na Utupatie mwongozo katika jambo letu (hili). Ee Mlezi wangu, Unipanulie kifua changu na Unirahisishie kazi yangu (hii).

**(34)**

***Dua baada ya kufanikiwa kazini***

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ الَّذِىْ بِنِعْمَتِهٖ تَتِمُّ الصَّالِحَاتُ۔

Tafsiri

Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu Ambaye kwa neema Yake hutimia (matendo) mema.

**(35)**

***Dua wakati wa kutofaulu kazini***

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَلٰى كُلِّ حَالٍ

Tafsiri

Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu kwa kila hali.

**(36)**

***Dua wakati wa kupata hasara kazini***

عَسٰى رَبُّنَا اَنْ يُّبْدِلَنَا خَيْرًا مِّنْهَا اِنَّا اِلٰى رَبِّنَا رَاغِبُوْنَ

Tafsiri

Huenda Mola wetu Atatubadilishia lililo bora kuliko hili; hakika sisi twamwomba Mola wetu kwa unyenyekevu.

**(37)**

***Dua wakati wa kuona jambo lichukizalo***

اَللّٰهُمَّ لَا يَأْتِىْ بِالْحَسَنَاتِ اِلَّآ اَنْتَ وَلَا يَدْفَعُ السَّيِّاٰتِ اِلَّآ اَنْتَ وَلَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ اِلَّا بِاللّٰهِ ـ

Tafsiri

Ee Mola wangu hakuna mwenye kuleta mema ila Wewe, wala hakuna aondoaye maovu ila Wewe; wala hakuna kinga wala nguvu ila hutoka kwa Mwenyezi Mungu.

**(38)**

***Dua wakati wa kuona kilema au mgonjwa***

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ الَّذِىْ عَافَانِىْ مِمَّا ابْتِلَاكَ بِهٖ وَفَضَّلَنِىْ

عَلٰى كَثِيْرٍ مِمَّنْ خَلَقَ تَفْضِيْلاً ـ

Tafsiri

Sifa zote njema ni Mwenyezi Mungu Aliyeniepusha na hayo ambayo Amekujaribu kwayo na Akanifadhili kuliko viumbe vyake vingi.

**(39)**

***Dua ipigapo radi***

اَلـلّٰهُـمَّ لَا تَقْتُلْنَا بِغَضَبِكَ وَلَا تُهْلِكْنَا بِعَذَابِكَ وَعَافِنَا قَبْلَ ذَالِكَ ـ

Tafsiri

Ee Mola wetu, Usituue kwa ghadhabu Yako, wala Usituangamize kwa adhabu Yako, na Utusamehe kabla ya hayo.

**(40)**

***Dua ya kuombea mvua yenye manufaa***

١ = اَللّٰهُمَّ سُقْيًا نَافِعًا

٢ = اَللّٰهُمَّ اجْعَلْهُ سَبَبَ رَحْمَةٍ وَلَا تَجْعَلْهُ سَبَبَ عَذَابٍ ـ

Tafsiri

Ee Mola wetu, Usituue kwa ghadhabu Yako, wala Usituangamize kwa adhabu Yako, na Utusamehe kabla ya hayo.

**(41)**

***Dua ya kuzuia mvua ikiwa imepita kiasi***

اَللّٰهُمَّ حَوَالَيْنَا وَلَا عَلَيْنَا ـ اَللّٰهُمَّ عَلَى الْآكَامِ وَالظِّرَابِ وَالْجِبَالِ وَبُطُوْنِ الْاَوْدِيَة وَمَنَابِتِ الشَّجَرَةِ

Tafsiri

Ee Mola wetu, Usitunyeshee (mvua hii), bali kandoni kwetu. Ee Mola wetu, (ipeleke) juu ya vichuguu na vilima na milima na sehemu za mabondeni na misituni.

**(42)**

***Dua wakati wa dhoruba kali***

اَللّٰهُمَّ اِنِّیۡ اَسۡأَلُكَ خَيۡرَ هٰذِهِ الرِّيَاحِ وَخَيۡرَ مَا فِيۡهَا وَخَيۡرَ مَآ اُرۡسِلَتۡ بِهٖ وَاَعُوۡذُ بِكَ مِنۡ شَرِّ مَا فِيۡهَا وَشَرِّ مَآ اُرۡسِلَتۡ بِهٖ ۔

Tafsiri

Ee Mola wangu, nakuomba heri ya pepo hizi na heri ya vilivyomo ndani yake na heri ya shabaha ya kupelekwa kwake; na ninakuomba Unilinde na shari ya vilivyomo ndani yake na shari ya shabaha ya kupelekwa kwake.

**(43)**

***Dua ya kuondolewa na hasira***

اَللّٰهُمَّ اغۡفِرۡ لِیۡ ذَنۡبِیۡ وَاَذۡهِبۡ غَيۡظَ قَلۡبِیۡ وَاَجِرۡنِیۡ مِنَ الشَّيۡطٰنِ الرَّجِيۡمِ ۔

Tafsiri:

Ee Mola wangu, Nighofirie dhambi zangu na Uondoe hasira moyoni mwangu na Uniokoe na shetani arujumiwaye.

(44)

***Dua ya kumuombea mtu anapokutumikia au anapokupa zawadi***

Mwenye kupokea zawadi au kutunukiwa atasema:

جَزَاكَ اللّٰهُ خَيْرًا۔

Yaani:

Mwenyezi Mungu Akulipe malipo mema.

Mwenye kutoa zawadi atajibu:

بَارَكَ اللّٰهُ لَكَ

Yaani Mwenyezi Mungu akubariki.

**(45)**

***Dua wakati wa kula matunda mapya***

١ = اَللّٰهُمَّ بَارِكْ لَنَا فِىْ ثَمَرِنَا وَ بَارِكْ لَنَا فِىْ مَدِيْنَتِنَا وَ بَارِكْ لَنَا فِىْ صَاعِنَا وَ بَارِكْ لَنَا فِىْ مُدِّنَا۔

٢ = اَللّٰهُمَّ كَمَآ اَرَيْتَنَآ اَوَّلَهٗ فَاَرِنَا اٰخِرَهٗ۔

Tafsiri:

1. Ee Mola wetu, Utubarikie matunda yetu na mji wetu na vyombo vyetu vya kupimia nafaka na matunda.
2. Ee Mola wetu, kama Ulivyotuonyesha sehemu yake ya mwanzo, Utuonyeshe sehemu yake ya mwisho.

**(46)**

***Dua wakati wa kusikia habari njema***

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ

Tafsiri:

Sifa zote njema Anazo Mwenyezi Mungu.

**(47)**

***Dua wakati wa kusikia msiba wa mtu au habari mbaya***

اِنَّا لِلّٰهِ وَاِنَّآ اِلَيْهِ رَاجِعُوْنَ۔

Tafsiri:

Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake tutarejea.

**(48)**

***Dua ya kupokea hukumu ya Mwenyezi Mungu kwa furaha***

اَلْـحَـمْـدُ لِـلّٰهِ عَلٰى كُلِّ حَالٍ وَاَعُوْذُ بِا للّٰهِ مِنْ حَالِ اَهْلِ النَّارِ۔

Tafsiri:

Mwenyezi Mungu Asifiwe kwa kila hali. Ninamkimbilia Mwenyezi Mungu aniokoe na hali ya watu wa Motoni.

**(49)**

***Dua ya kuokolewa na shari ya maadui***

١ = اَللّٰهُمَّ اِنَّا نَجْعَلُكَ فِىْ نُحُوْرِهِمْ وَنَعُوْذُبِكَ مِنْ شُرُوْرِهِمْ۔

٢ = رَبِّ كُلُّ شَىْءٍ خَادِمُكَ ــ رَبِّ فَاحْفَظْنَا وَانْصُرْنَا وَارْحَمْنَا۔

٣ = يَا حَفِيْظُ يَا عَزِيْزُ يَا رَفِيْقُ۔

Tafsiri:

1. Ee Mola wetu, tunakuweka mbele ya vifua vyao (maadui wetu, Ushindane nao) na twakuomba Utulinde na shari zao.

2. Ee Mola wangu, kila kitu kinatii amri Yako, basi Utulinde na Utunusuru na Uturehemu.

3. Ee Mlinzi - Ee Mwenye nguvu - Ee Mwenzi (Unisaidie).

## (50)

***Dua wakati wa hofu au msukosuko***

١ = اَللّٰهُمَّ اسْتُرْ عَوْرَاتِنَا وَاٰمِنْ رَوْعَاتِنَا ـ

٢ = يَا حَيُّ يَا قَيُّوْمُ بِرَحْمَتِكَ اَسْتَغِيْثُ ـ

٣ = اَللّٰهُمَّ رَحْمَتَكَ اَرْجُوْا فَلَا تَكِلْنِىْ اِلٰى نَفْسِىْ طُرْفَةَ عَيْنٍ وَاصْلِحْ شَأْنِىْ كُلَّهٗ لَآ اِلٰهَ اِلَّا اَنْتَ ـ

٤ = لَآ اِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ الْعَظِيْمُ الْحَكِيْمُ ـ لَآ اِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ رَبُّ الْعَرْشِ الْعَظِيْمِ ـ لَآ اِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ رَبُّ السَّمٰوٰتِ وَرَبُّ الْاَرْضِ وَرَبُّ الْعَرْشِ الْكَرِيْمِ ـ

Tafsiri:

1. Ee Mola wetu, Utusitiri aibu zetu na Uondoe hofu zetu.

2. Ee Mwenye uzima - Ee Mhifadhi wa milele - Unisaidie kwa huruma Yako.

3. Ee Mola wangu, nataraji rehema Yako; basi

Usiniache peke yangu hata kwa muda wa kupepesa macho. Na Unitengenezee jambo langu lote; hakuna aabudiwaye ila Wewe tu.

4. Hapana apasaye kuabudiwa ila Mwenyezi Mungu Mwenye adhama, Mwenye hekima. Hapana apasaye kuabudiwa ila Mwenyezi Mungu, Mwenye kiti cha Enzi Tukufu. Hapana apasaye kuabudiwa ila Mwenyezi Mungu, Mola wa mbingu na ardhi na Mola wa kiti cha Enzi chenye heshima.

**(51)**

***Dua wakati wa kukumbana na adui vitani***

اَللّٰهُمَّ اَنْتَ عَضُدِىْ وَنَصِيْرِىْ بِكَ اَحُوْلُ وَبِكَ اَصُوْلُ وَبِكَ اُقَاتِلُ

Tafsiri:

Ee Mola wangu, Wewe ndiwe mkono wangu na Msaidizi wangu; kwa msaada Wako ninatembea, na kwa nguvu Yako nashambulia na kwa nusura Yako napigana.

## (52)

***Dua ya kutaka kujizuia na maasi na kuomba baraka katika maungo na kuingizwa peponi na kulindwa na shari za maadui***

اَللّٰهُمَّ اقْسِمْ لَنَا مِنْ خَشْيَتِكَ مَا تَحُوْلُ بِهٖ بَيْنَنَا وَبَيْنَ مَعَاصِيْكَ وَمِنَ الْيَقِيْنِ مَا تُهَوِّنُ بِهٖ عَلَيْنَا جَنَّتَكَ وَاَللّٰهُمَّ يَارَبَّنَا مَتِّعْنَا بِاَسْمَاعِنَا وَاَبْصَارِنَا وَقُوَّتِنَا مَااَحْيَيْتَنَا وَاجْعَلْهُ الْوَارِثَ مِنَّا ـ اَللّٰهُمَّ اجْعَلْ ثَأْرَنَا عَلٰى مَنْ ظَلَمَنَا وَانْصُرْنَا عَلٰى مَنْ عَادَانَا ـ

Tafsiri:

Ee Mola wetu, Utugawie hofu Yako ambayo kwayo Utaingia kati yetu na kati ya maasi yetu; na Utugawiye katika yakini (juu ya dhati Yako na nguvu Zako) ambayo kwayo Utatupatia Pepo Yako kwa urahisi.

Na ee Mola wetu na Mlezi wetu, Utunufaishe kwa masikio yetu na macho yetu na nguvu zetu

maisha yetu yote. Na mrithi wetu awe mwanakwetu. Ee Mola wetu, Utuwezeshe kujilipiza kisasi kwa yule aliyetudhulumu na Utusaidie juu ya adui zetu.

**(53)**

***Dua wakati wa kutoka nyumbani kwa ajili ya safari***

بِسْمِ اللّٰهِ تَوَكَّلْتُ عَلَى اللّٰهِ وَلَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ اِلَّا بِاللّٰهِ ـــ اَللّٰهُمَّ اِنِّيْٓ اَعُوْذُبِكَ اَنْ اَضِلَّ اَوْ اُضَلَّ اَوْ اَظْلِمَ اَوْ اُظْلَمَ اَوْ اَجْهَلَ اَوْ يُجْهَلَ عَلَيَّ۔

Tafsiri:

(Natoka) kwa jina la Mwenyezi Mungu.

Namtegemea Mwenyezi Mungu (tu).

Hakuna kinga wala nguvu ila Kwake Mwenyezi Mungu. Ee Mola wangu, nakimbilia Kwako nijilinde na kupotea au kupotezwa, au kudhulumu au kudhulumiwa, au kufanya au kufanyiwa ujinga.

**(54)**

***Dua ya kuagana na mtu***

اَسْتَوْدِعُ اللّٰهَ دِيْنَكَ وَاَمَانَتَكَ وَاٰخِرَعَمَلِكَ ـ زَوَّدَكَ اللّٰهُ التَّقْوٰى وَغَفَرَ ذَنْبَكَ وَيَسَّرَ لَكَ الْخَيْرَ حَيْثُ مَا كُنْتَ ـ

Tafsiri:

Naweka katika ulinzi wa Mwenyezi Mungu dini yako na uaminifu wako na mwisho wa matendo yako. Mwenyezi Mungu Akutunukie utawa na Afunike dhambi zako na Akurahisisishie kupata heri popote ulipo.

**(55)**

***Dua nyingine za kwenda safari***

١ = اَللّٰهُمَّ اَنْتَ الصَّاحِبُ فِيْ السَّفَرِ وَالْخَلِيْفَةُ فِيْ الْاَهْلِ ـ

٢ = اَللّٰهُمَّ اِنِّيْ اَعُوْذُبِكَ مِنْ وَعْثَاءِ السَّفَرِ وَ كَابَةِ

الْـمُـنْقَلَبِ وَالْحَوْرِ بَعْدَ الْكَوْرِ وَدَعْوَةِ الْمَظْلُوْمِ وَسُوْٓءِ
الْمَنْظَرِ فِىْ الْمَالِ وَالْاَهْلِ ۔

٣ = اَللّٰهُمَّ اِنَّا نَسْئَلُكَ فِىْ سَفَرِنَا هٰذَاالْبِرَّ وَالتَّقْوٰى
وَمِنَ الْعَمَلِ مَا تَرْضٰى ۔ اَللّٰهُمَّ هَوِّنْ عَلَيْنَا سَفَرَنَا هٰذَا
وَاَطْوِ عَنَّا بُعْدَهٗ ۔

Tafsiri:

1. Ee Mola wetu, Wewe Ndiwe Mwenzi safarini na Mlinzi katika ahali (zangu).

2. Ee Mola wangu, ninakuomba Unilinde na taabu za safari nisione hali mbaya. Na Unilinde nisipate hasara baada ya faida, na Unilinde na maapizo ya mwenye, kudhulumiwa, na Unilinde na jicho baya katika mali yangu na ahali zangu.

3. Ee Mola wetu, tunakuomba wema na utawa katika safari yetu hii, Utuwezeshe kutenda matendo Unayoyapenda. Ee Mola wetu, Uturahishie safari yetu hii na Utufupishie umbali wake.

**(56)**

***Dua wakati wa kupanda kitu cha kusafiria, meli au gari na kadhalika***

اَللّٰهُ اَكْبَرُ ـ اَللّٰهُ اَكْبَرُ ـ اَللّٰهُ اَكْبَرُ ـ سُبْحَانَ الَّذِىْ سَخَّرَ لَنَا هٰذَا وَمَا كُنَّا لَهٗ مُقْرِنِيْنَ ـ وَاِنَّآ اِلٰى رَبِّنَا لَمُنْقَلِبُوْنَ ـ

Tafsiri:

Mwenyezi Mungu ni Mkuu kuliko wote; Mwenyezi Mungu ni Mkuu kuliko wote; Mwenyezi Mungu ni Mkuu kuliko wote. Atukuzwe Yeye Aliyetutiishia hii (au huyu, au hili au hiki na kadhalika). Ambapo sisi tusingaliweza kuitiisha kwa nguvu yetu; na bila shaka sisi ni wenye kurudia kwa Mola wetu.

**(57)**

***Dua wakati wa kushuka ndani ya gari, chombo au ndege***

بِسْمِ اللّٰهِ مَجْرٖ ىهَا وَمُرْسٰهَا اِنَّ رَبِّىْ لَغَفُوْرٌ رَّحِيْم۔

Tafsiri:

Kwa jina la Mwenvezi Mungu kuwe kwenda kwake na kusimama kwake. Hekika Mola wangu ni Msamehevu, Mrehemevu.

**(58)**

***Dua wakati wa kupanda palipoinuka kama kilima au mlima***

اَللّٰهُمَّ لَكَ الشَّرَفُ عَلٰى كُلِّ شَرَفٍ وَلَكَ الْحَمْدُ عَلٰى كُلِّ حَالٍ۔

Tafsiri:

Ee Mola wetu, heshima Yako iko juu kuliko kila aliye juu na tunakusifu kwa hali yoyote ile.

## (59)

***Dua wakati wa kuteremka kutoka palipoinuka***

١ = اٰئِبُوْنَ تَـآئِبُوْنَ عٰبِدُوْنَ لِرَبِّنَا حَامِدُوْنَ ـ

٢ = تَوُبًا تَوُبًا لِرَبِّنَا اَوُبًا لَا يُغَادِرُ عَلَيُنَا حُوُبًا ـ

Tafsiri:

1. (Sisi ni) wenye kurejea, wenye kutubu, wenye kumwabudu Mola wetu na wenye kumsifu.

2. Tunatubu na kutubu tena na tena; tunarejea kwa Mola wetu, Naye Haachi juu yetu dhambi hata moja (Anatusamehe zote).

## (60)

***Dua wakati wa kuingia kijiji au mji***

اَللّٰهُـمَّ اِنَّا نَسُئَلُكَ خَيُرَ هٰذِهِ الُقَرُيَةِ وَخَيُرَ اَهُلِهَا وَخَيُرَ مَـا فِيُهَـا وَنَـعُوُذُبِكَ مِنُ شَرِّ هٰذِهِ الُقَرُيَةِ وَ شَرِّ اَهُلِهَا وَشَرِّمَا فِيُهَا ـ

اَللّٰهُمَّ ارْزُقْنَا جَنَاهَا وَحَبِّبْنَا اِلٰى اَهْلِهَا وَحَبِّبْ صَالِحِىْ اَهْلِهَا اِلَيْنَا ـ

Tafsiri:

Ee Mola wetu, twakuomba heri ya kijiji hiki (au mji huu) na heri ya wakazi wake na heri ya yote yaliyomo ndani yake; na twakuomba Utulinde na shari ya kijiji hiki na shari ya wakazi wake na shari ya yaliyomo ndani yake. Ee Mola wetu, Utubarikie humo.

Ee Mola wetu, Uturuzuku matunda yake na Utufanye tuwe vipenzi wa wakazi wake na Utufanye tupendane na watu wake walio wema.

**(61)**

***Dua baada ya kurejea kutoka safari***

اَللّٰهُمَّ اِنِّىْ اَسْأَلُكَ خَيْرَ الْمُوْلَجِ وَخَيْرَ الْمَخْرَجِ بِسْمِ اللّٰهِ وَلَجْنَا وَعَلَى اللّٰهِ رَبِّنَا تَوَكَّلْنَا ـ

Tafsiri:

Ee Mola wangu, nakuomba heri ya kuingia (nyumbani) na heri ya kutoka humo.

Kwa jina la Mwenyezi Mungu tunaingia na Kwake Mwenyezi Mungu, Mola wetu, tunategemea.

**(62)**

***Dua wakati wa kutoka katika mkutano***

سُبْحَانَكَ اللّٰهُمَّ وَبِحَمْدِكَ - اَشْهَدُ اَنْ لَّا اِلٰهَ اِلَّآ اَنْتَ اَسْتَغْفِرُكَ وَاَتُوْبُ اِلَيْكَ -

Tafsiri:

Utakatifu ni Wako, ee Mola wangu, na sifa njema ni Zako. Nashuhudia kwamba hapana anayestahili kuabudiwa ila Wewe; nakuomba msamaha na kutubia Kwako.

**(63)**

***Dua ya kutoa shukurani juu ya neema za Mwenyezi Mungu na kuomba kupewa zaidi.***

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ الَّذِيْ كَفَانِىْ وَاٰوَانِىْ وَ اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ الَّذِيْ اَطْعَمَنِىْ وَسَقَانِىْ وَ الْحَمْدُ لِلّٰهِ الَّذِيْ مَنَّ عَلَيَّ۔ اَسْأَلُكَ اَنْ تُجِيْرَنِىْ مِنَ النَّارِ۔

Tafsiri:

Namsifu Mwenyezi Mungu Aliyenitosheleza na Akanikalisha (pema). Namshukuru Mwenyezi Mungu Aliyenilisha na kuninywesha na kumsifu juu ya hisani Alizonifanyia. (Ee Mola wangu) ninakuomba Uniokoe na Moto.

**(64)**

***Dua ya kuomba uimara***

اَللّٰهُمَّ ثَبِّتْ قَلْبِىْ عَلٰى دِيْنِكَ۔

Tafsiri:

Ee Mola wangu, Uniimarishe moyo wangu juu ya dini Yako.

**(65)**

***Dua ya kuwaombea bwana na bibi arusi***

بَارَكَ اللّٰهُ لَكَ بَارَكَ اللّٰهُ لَكَ وَ بَارَكَ عَلَيْكُمَا وَجَمَعَ بَيْنَكُمَا فِى الْخَيْرِ ۔

Tafsiri:

Mwenyezi Mungu Akubariki, Mwenyezi Mungu Akubariki na Akubarikini wote wawili na Awakutanisheni pamoja kwa heri.

**(66)**

***Dua ya kuombwa na bwana arusi kwa ajili ya mkewe***

اَللّٰهُمَّ اِنِّىْ اَسْأَلُكَ مِنْ خَيْرِهَا وَخَيْرِ مَا جَبَلْتَهَا عَلَيْهِ وَاَعُوْذُ بِكَ مِنْ شَرِّهَا وَشَرِّ مَا جَبَلْتَهَا عَلَيْهِ ۔

Tafsiri:

Ee Mola wangu, nakuomba heri yake na heri ya tabia Uliyomwumba nayo; na nakuomba Unilinde na shari yake na shari ya tabia Uliyomwumba nayo.

**(67)**

***Dua inayotakiwa kusomwa an mume na mke wanapokuwa kitanda kimoja***

بِسْــمِ اللّٰهِ اَللّٰهُمَّ جَنِّبْنَا الشَّيْطٰنَ وَجَنِّبِ الشَّيْطٰنَ مَا رَزَقْتَنَا۔

Tafsiri:

(Tunakutana) kwa jina la Mwenyezi Mungu. Ee Mola wetu, Utuepushe na shetani na Umwepushe na shetani yule (mtoto) Utakayetupa.

**(68)**

***Dua ya kuwaombea wagonjwa na kupata afya***

١ = اَلـلّٰهُـمَّ رَبَّ الـنَّـــاسِ اَذْهِبِ الْبَـاْسَ اِشْفِ اَنْتَ

الشَّافِىُ لَا شِفَـاءَ اِلَّا شِفَآئُكَ شِفَـاءً لَّا يُغَادِرُ سَقَمًا

٢ = بِسْـمِ اللّٰـهِ الْكَافِىُ ـ بِسْمِ اللّٰهِ الشَّافِىُ بِسْمِ اللّٰهِ الْغَفُوْرُ الرَّحِيْمِ ـ بِسْمِ اللّٰهِ الْبَرِّ الْكَرِيْمِ ـ يَا وَلِىُّ اشْفِنَا

٣ = اَللّٰـهُـمَّ عَـافِـنِـىْ فِـىْ بَـدَنِـىْ اَللّٰهُمَّ عَافِنِىْ فِىْ سَـمْـعِىْ اَللّٰـهُـمَّ عَافِنِىْ فِىْ بَصَرِىْ لَآ اِلٰهَ اِلَّا اَنْتَ ـ اَللّٰـهُـمَّ اِنِّـىْ اَعُـوْذُبِكَ مِـنَ الْكُفْرِ وَالْفَقْرِ اَللّٰهُمَّ اِنِّىْٓ اَعُوْذُبِكَ مِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ لَآ اِلٰهَ اِلَّا اَنْتَ ـ

Tafsiri:

1. Ee Mola wetu, Mlezi wa watu wote, Uondoe shida na Uponye, Wewe Ndiye Mponyeshaji wala hakuna nafuu ila ile inayotoka Kwako. Ulete nafuu isiyobakisha kasoro.

2. Kwa jina la Mwenyezi Mungu Anayetosheleza kwa jina la Mwenyezi Mungu Anayeponya - kwa jina la Mwenyezi Mungu Msamehevu, Mrehemevu - kwa jina la Mwenyezi Mungu

Mwema, Mpole. Ee Mlinzi, Utuponye.

3. Ee! Mola wetu, nipe afya mwilini mwangu; Ee! Mola wetu, nipe afya masikioni mwangu; Ee! Mola wetu, nipe afya katika kuona kwangu. Hakuna aabudiwaye kwa haki ila Wewe. Ee! Mola wetu, najilinda Kwako na kufuru na njaa. Ee! Mola wetu, najilinda Kwako na adhabu ya kaburi, hakuna apasaye kuabudiwa ila Wewe.

**(69)**

***Dua afapo mtu***

١ = اِنَّا لِلّٰهِ وَاِنَّآ اِلَيْهِ رَاجِعُوْنَ اَللّٰهُمَّ اَجِرْنِىْ فِىْ مُصِيْبَتِىْ وَاخْلُفْ لِىْ خَيْرًا مِّنْهَا ـ

اَللّٰهُمَّ اغْفِرْلِ ....... وَارفَعْ دَرَجَتَهٗ فِى الْمَهْدِيِّيْنَ وَخْلِفْهُ فِىْ عَقِبِهٖ فِىْ الْغَابِرِيْنَ وَاغْفِرْ لَنَا وَلَهٗ يَا رَبَّ الْعٰلَمِيْنَ وَافْسَحْ لَهٗ فِىْ قَبْرِهٖ وَنَوِّرْ لَهٗ ـ

Tafsiri

1 . Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, Kwake tutarejea. Ee Mola wangu, Unipe ujira katika msiba wangu na Unibakishie kile kilicho bora kuliko hiki.

2. Ee Mola wangu, Umsamehe (litajwe hapa jina la marehemu) na Umnyanyue cheo chake katika wale walioongoka na Umwekee warithi katika waliosalia nyuma yake, na Utusamehe sisi, na yeye (pia), ee Mola wa Walimwengu, na Umpanulie kaburi lake na Umwekee nuru ndani yake.

**(70)**

***Dua ya kusomwa na yule anayefika mahali alipowekwa maiti***

اَللّٰهُمَّ اغْفِرْلِىْ وَلَهٗ اِنَّ رَبِّىْ لَغَفُوْرٌ رَّحِيْمٌ

Tafsiri:

Ee Mola wetu, Nighofirie mimi na yeye (pia); hakika Mola wangu ni Msamehevu. Mrehemevu.

**(71)**

***Dua wakati wa kumfumba macho marehemu na kumlaza kaburini***

بِسْمِ اللّٰهِ وَعَلٰى مِلَّةِ رَسُوْلِ اللّٰهِ ۔

Tafsiri:

Kwa jina la Mwenyezi Mungu na kwa desturi ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w).

**(72)**

***Dua wakati wa kupita makaburini***

١ = اَلسَّلَامُ عَلَيْكُمْ اَهْلَ الدِّيَارِ مِنَ الْمُؤْمِنِيْنَ وَالْمُسْلِمِيْنَ وَاِنَّا اِنْ شَآءَ اللّٰهُ بِكُمْ لَلَاحِقُوْنَ ۔ نَسْأَلُ اللَّهَ لَنَا وَلَكُمُ الْعَافِيَة ۔

٢ = اَلسَّلَامُ عَلَيْكُمْ يَا اَهْلَ الْقُبُوْرِ يَغْفِرُ اللّٰهُ لَنَا وَلَكُمْ اَنْتُمْ سَلَفُنَا وَنَحْنُ بِالْاَثَرُ ۔

Tafsiri:

1. Amani iwe juu yenu, enyi wakazi wa nyumba hili miongoni mwa waaminio na Waislamu, na hakika sisi (pia), Akipenda Mwenyezi Mungu, tutakuja kukutana nanyi. Twamuomba Mwenyezi Mungu Atuondolee shida sisi na ninyi (pia).

2. Amani iwe juu yenu enyi wenye makaburi. Mwenyezi Mungu Atusamehe sisi na ninyi pia. Ninyi mmetutangulia na sisi tunafuata nyayo zenu.

**(73)**

***Dua ya kunuia Haji (Husomwa baada ya kuoga na kuvaa ihram na kusali rakaa mbili)***

اَللّٰهُمَّ اِنِّىْ اُرِيْدُ الْحَجَّ فَتَقَبَّلْ مِنِّىْ وَيَسِّرْهُ لِىْ ۔

Tafsiri:

Ee Mola wangu, nakusudia kufanya haji, basi Nitakabalie na Nirahisishie (ibada hiyo).

**(74)**

***Talbiya au dua ya kusomwa nyakati zote za faragha katika kuhiji Makka Mukarramah.***

اَللّٰهُمَّ لَبَّيْكَ لَبَّيْكَ لَا شَرِيْكَ لَكَ لَبَّيْكَ اِنَّ الْحَمْدَ وَالنِّعْمَةَ لَكَ وَالْمُلْكَ لَكَ وَلَا شَرِيْكَ لَكَ ـ اَللّٰهُ اَكْبَرُ لَآ اِلٰـهَ اِلَّا اللّٰهُ ـ

Tafsiri:

Ee Mola wangu, labeka (nipo hapa mbele Yako kwa kukutumikia na kukutii) labeka. Huna mshirika labeka. Hakika sifa zote njema na neema zote ni Zako, na Ufalme pia ni Wako, wala Huna mshirika. Mwenyezi Mungu ni Mkuu kabisa. Hapana apasaye kuabudiwa ila Mwenyezi Mungu.

**(75)**

***Dua wakati wa kuzunguka Ka'aba***

سُبْحَانَ اللّٰهِ وَالْحَمْدُ لِلّٰهِ وَلَآ اِلَـهَ اِلَّا اللّٰهُ ـ اَللّٰهُ اَكْبَرُ

وَلَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ اِلَّا بِاللّٰهِ۔

Tafsiri:

Utakatifu ni wa Mwenyezi Mungu na sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu.

Hakuna anayestahili kuabudiwa ila Allah. Allah ni Mkuu kabisa; na hakuna kinga ila Anayo Mwenyezi Mungu.

**(76)**

***Dua wakati wa kukurubia nguzo inayoitwa Arrukn-ul-yamaani katika Kuhiji.***

اَللّٰهُمَّ اِنِّيْٓ اَسْأَلُكَ الْعَفْوَ الْعَافِيَةَ فِىْ الدُّنْيَا وَالْاٰخِرَةِ۔ رَبَّنَا اٰتِنَا فِىْ الدُّنْيَا حَسَنَةً وَّفِىْ الْاٰخِرَةِ حَسَنَةً وَّقِنَا عَذَابَ النَّارِ۔

Tafsiri:

Ee Mola wetu, ninakuomba msamaha na afya katika dunia na Akhera. Ee Mola wetu, Utupe mema katika dunia na mema katika Akhera na Utuokoe na adhabu ya Moto.

**(77)**

***Dua wakati wa kukimbia baina ya vilima viwili vya Safaa na Marwah katika Haji.***

رَبِّ اغْفِرْ وَارْحَمْ اَنْتَ الْاَعَزُّ الْاَكْرَمُ ۔

Tafsiri:

Ee Mola wangu, Unighofirie na Unirehemu. Wewe ni Mwenye nguvu na Mwenye heshima kuliko wote.

**(78)**

***Dua wakati wa kushinda katika uwanja wa Arafaat siku ya Haji.***

١ = لَآ اِلٰــهَ اِلَّا اللّٰهُ وَحْدَهٗ لَا شَرِيْكَ لَهٗ ۔ لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ وَهُوَ عَلٰى كُلِّ شَىْءٍ قَدِيْرٌ ۔

٢ = اَللّٰهُمَّ اهْدِنَا بِالْهُدٰى وَزَيِّنَّا بِالتَّقْوٰى وَاغْفِرْ لَنَا فِىْ الْاٰخِرَةِ وَالْاُوْلٰى ۔ اَللّٰهُمَّ اِنِّىْ اَسْأَلُكَ رِزْقًا حَلَالًا

طَيِّبًا مُّبَارَكًا اَللّٰهُمَّ مَا اَحْبَبْتَ مِنْ خَيْرٍ فَحَبِّبْهُ اِلَيْنَا وَيَسِّرْ لَنَا وَمَا كَرِهْتَ مِنْ شَرٍّ فَكَرِّهْهُ اِلَيْنَا وَجَنِّبْنَاهُ وَلَا تَنْزِعْ مِنَّا الْاِسْلَامَ بَعْدَ اِذْ هَدَيْتَنَا ـ

Tafsiri:

1. Hakuna apasaye kuabudiwa ila Mwenyezi Mungu, hana mshirika. Ufalme ni Wake na sifa zote njema ni Zake, Naye ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

2. Ee Mola wetu, Utuongoze kwa mwongozo kamili na Utupambe kwa utawa na Utughofirie katika dunia na Akhera. Ee Mola wangu, nakuomba riziki iliyo halali na nzuri na yenye baraka. Ee Mola wetu, heri yoyote Unayoipenda, basi Utufanye na sisi tuwe wenye kuipenda na Uturahisishie heri hiyo; na shari yoyote Unayoichukia, basi Utufanye na sisi tuwe wenye kuichukia na Utuepushe nayo shari hiyo. Wala Usituondolee Uislamu baada ya kutuongoza (kwenye dini hiyo).

(79)

***Dua baada ya kumaliza kisomo cha Kurani Tukufu***

صَدَقَ اللّٰهُ صَدَقَ اللّٰهُ الْعَلِيُّ الْعَظِيْمُ ـ وَصَدَقَ رَسُوْلُهُ
النَّبِيُّ الْكَرِيْمُ وَنَحْنُ عَلٰى ذٰلِكَ مِنَ الشّٰهِدِيْنَ وَ
الشَّاكِرِيْنَ ـ اَللّٰهُمَّ ارْحَمْنِيْ بِالْقُرْاٰنِ الْعَظِيْمِ وَاجْعَلْهُ
لِيْ اِمَامًا وَّنُوْرًا وَّهُدًى وَّرَحْمَةً ـ اَللّٰهُمَّ ذَكِّرْنِيْ مِنْهُ
مَا نَسِيْتُ وَعَلِّمْنِيْ مِنْهُ مَا جَهِلْتُ وَارْزُقْنِيْ تِلَاوَتَهٗ
اٰنَاۤءَ اللَّيْلِ وَ النَّهَارِ وَاجْعَلْهُ لِيْ حُجَّةً يَّا رَبَّ الْعٰلَمِيْنَ ـ

Tafsiri:

Amesema kweli Mwenyezi Mungu. Amesema kweli Mwenyezi Mungu Aliye juu, Mkuu, na amesema kweli Mtume Wake Nabii mwenye heshima; nasi ni wenye kutoa ushahidi na shukurani (pia) juu ya jambo hili. Ee Mola wangu, Unirehemu kwa Kurani Tukufu na Uifanye iwe

kwangu kiongozi na nuru na mwongozo na rehema. Ee Mola wangu, Unikumbushe ya humo niliyoyasahau, na Unifundishe ya humo nisiyo yajua, na Uniruzuku (uwezo wa) kuisoma nyakati za usiku na mchana, na Uifanye iwe kwangu hoja, ee Mola wa Walimwengu.

**(80)**

***Dua ya Istikhara (kuomba heri kwa Mwenyezi Mungu katika kila jambo).***

اَللّٰهُمَّ اِنِّىٓ اَسْتَخِيْرُكَ بِعِلْمِكَ وَاَسْتَقْدِرُكَ بِقُدْرَتِكَ وَاَسْئَلُكَ مِنْ فَضْلِكَ الْعَظِيْمِ فَاِنَّكَ تَقْدِرُ وَلَا اَقْدِرُ وَتَعْلَمُ وَلَا اَعْلَمُ وَاَنْتَ عَلَّامُ الْغُيُوْبِ۔

اَللّٰهُمَّ اِنْ كُنْتَ تَعْلَمُ اَنَّ هٰذَا الْاَمْرَ خَيْرٌ لِّىْ فِىْ دِيْنِىْ وَمَعَاشِىْ وَعَاقِبَةِ اَمْرِىْ فَاقْدِرْهُ لِىْ وَيَسِّرْهُ لِىْ ثُمَّ بَارِكْ لِىْ فِيْهِ وَاِنْ كُنْتَ تَعْلَمُ اَنَّ هٰذَا الْاَمْرَ شَرٌّ لِّىْ فِىْ دِيْنِىْ وَمَعَاشِىْ وَعَاقِبَةِ اَمْرِىْ فَاصْرِفْهُ عَنِّىْ

وَاصْرِفْنِيْ عَنْهُ وَاقْدِرْلِيَ الْخَيْرَ حَيْثُ كَانَ ثُمَّ ارْضِنِيْ بِهٖ

Tafsiri:

Ee Mola wangu, hakika ninakuomba heri katika elimu Yako, na ninakuomba uwezo katika kudura Yako, na ninakuomba katika fadhili Zako kuu; maana Wewe Ndiye Uwezaye na mimi sina uwezo, na Wewe Ndiye Ujuaye na mimi sina ujuzi, na Wewe Ndiye Mjuzi wa mambo ya ghaibu. Ee Mola wangu, ikiwa Unafahamu ya kuwa jambo hili litakuwa la heri kwangu katika dini yangu na maisha yangu na matokeo yake ni mema kwa ajili yangu, basi nijaalie hili na nirahisisishie na tena nibarikie kwalo. Na ikiwa Unafahamu ya kuwa jambo hili lina shari kwangu katika dini yangu na maisha yangu na matokeo yake ni mabaya basi litenge mbali nami na Unitenge mbali nalo. Na Unijaalie jambo la heri po pate lipatikanapo, kisha Unifanye niridhike nalo.

**AMANI NA BARAKA ZA MWENYEZI MUNGU ZIWE JUU YA MTUME MUHAMMAD S.A.W.**